

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU-KAZI, AJIRA,  
VIJANA NA WENYE ULEMAVU**

**MHE. JENISTA MHAGAMA (MB), KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO CHA  
BARAZA LA WAFANYAKAKAZI WA WAKALA WA USALAMA NA  
AFYA MAHALI PA KAZI (OSHA), DODOMA, 02 DISEMBA, 2016**

Mtendaji Mkuu wa OSHA

Wakurugenzi,

Mameneja

Wakuu wa Vitengo na

Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la OSHA

Asalam alekum.....

Tumsifu Yesu Kristo.....

Bwana Yesu Asifiwe.....

Nianze kwakumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ni mwingi wa rehema kwakutujalia sote hapa afya njema na kutuwezesha kukutana mahali hapa kwaajili ya kikao cha sita (6) cha Baraza la Pili la Wafanyakazi wa OSHA.

Nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mtendaji Mkuu pamoja na menejimenti nzima ya Wakala kwa kunikaribisha kuwa Mgeni Rasmi katika ufunguzi wa kikao hiki muhimu ambacho mnakutana kutathmini utendaji wenu na kuweka mikakati zaidi katika kuboresha kazi zenu.

Ndugu wafanyakazi, awali ya yote nianze kwakutambua kazi nzuri mnayoifanya katika kuimarisha hali ya usalama na afya kwa idadi kubwa ya

wafanyakazi wa sekta mbali mbali hapa nchini kwani taarifa zilizopo zinaonesha mafanikio yaliyofikiwa na taasisi yenu katika kutekeleza lengo mahususi la kuanzishwa kwake.

Miongoni mwa mafanikio hayo ni kuongezeka kwa idadi ya sehemu za kazi zilizosajiliwa na Wakala hadi kufikia zaidi ya 12,500 likiwa ni ongezeko la takribani sehemu za kazi 2,000 kutoka idadi ya mwaka uliopita. Kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi waliochunguzwa afya zao kutoka 15,418 kwa mwaka wa fedha 2007/8 hadi kufikia 66,889 katika mwaka wa fedha wa 2015/16.

Aidha kozi ya Taifa ya Afya na Usalama mahali pa kazi kwa maafisa wa usalama na afya mahali pa kazi imeanzishwa ambapo mpaka sasa idadi ya wahitimu hao imefikia zaidi ya 1,800. Wakala umeratibu uridhiaji wa mikataba ya Afya na usalama mahali pa kazi ya ILO ipatayo sita (6) na kutunga kanuni nne (4) za Afya na Usalama hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha wa 2015/16. Aidha katika kipindi kifupi cha mwaka huu wa fedha tayari kanuni mbili zimesainiwa na kufanya kanuni ziwe 6.

Mafanikio mengine ni uboreshaji wa maslahi kwa watumishi kwa kuweka vivutio vya maslahi (incentive scheme), kutoa chai na chakula cha mchana pamoja na kuanzisha program ya mazoezi ya kujenga miili kwa watumishi.

Wakala umezindua mkataba wa huduma bora kwa mteja tangu mwaka wa fedha 2013/14 na kutoa mafunzo ya huduma bora kwa mteja kwa watumishi wote.

Wakala umefanikiwa kuongeza vitendea kazi na nyenzo nyingine ambazo zimewawezesha kusogeza huduma kwa wananchi kwa kufungua ofisi

mikoani kufikia uwepo wa ofisi za OSHA katika mikoa 10 hadi sasa, na ofisi tatu nyingine ziko mbioni kufunguliwa.

Ndugu wafanyakazi, hayo ni baadhi tu ya mafanikio katika mengi ambayo taasisi yenu imeyapata katika kipindi cha hivi karibuni.

Siku zote tunasema palipo na mafanikio huwa hapakosi changamoto ambapo changamoto mbalimbali zimekuwa zikijitokeza katika kutekeleza majukumu ya Wakala kama vile idadi isiyotosha ya watumishi ukilinganisha na mahitaji ya nchi. Ufinyu wa majengo ya Ofisi, Kudorola kwa hali ya Afya na Usalama katika sekta ya wajasiriamali kwani hawamudu kulipia gharama za ukaguzi na mafunzo ya Usalama na Afya. Halikadhalika bado kuna uelewa mdogo wa masuala ya Afya na Usalama miongoni mwa wadau wetu.

Ndugu wafanyakazi, ni matumaini yangu kwamba kikao kazi hiki kitajikita sasa katika kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto tajwa ambazo kama zisiposhughulikiwa kikamilifu zinaweza kukwamisha utekelezaji wa dira ya taasisi yetu ambayo ni kuhakikisha kwamba sehemu za kazi zinakuwa na hali nzuri kiusalama na kiafya.

Mwisho ningependa kuwakumbusha kuzingatia falsafa ya serikali ya awamu ya tano ya kujenga uchumi wa viwanda na kuwahimiza wananchi kufanya kazi. Hivyo huduma zetu zinazohusu masuala ya Usalama na Afya mahali pa Kazi ni lazima zilenge kuisaidia serikali kutimiza azma yake kwa kutoa huduma zenye viwango stahiki na zenye mwelekeo wa kuchochea uchumi wa viwanda katika nchi yetu.

Baada ya kusema hayo, natamka kwamba kikao hiki kimefunguliwa rasmi na niwatakie mafanikio mema katika kazi hii muhimu.

Asanteni kwakunisikiliza